# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la kwanza na la pili

Mfululizo wa A
Masomo ya kwanza hadi sita

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya “Wakati na Biblia/Bibletime”, “Maisha Mapya/New Life” na “Wakusanyaji/Gleaners” kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wamechukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wakufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa na vikundi mbalimbali kutoka makanisa na shule mbalimbali ambavyo vimezingatia mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na yanamruhusu mwanafunzi kuyatumia kwa muda mrefu hadi atakapotimiza umri wa miaka ishirini. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (chini ya miaka mitano), miaka mitano hadi saba, miaka nane hadi kumi, miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu na miaka kumi na minne hadi kumi na sita. Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 6). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongonzo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwa mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES

**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo wa kufundisha umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo wa kufundisha katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya daraja la kwanza na la pili kwa watoto wenye umri wa wastani wa miaka 5-10.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kwa kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Hatupendi kutoa shinikizo na kutokuwapa waalimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri –** Waalimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza –** Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno 'Tunajifunza kuwa' ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Waalimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi –** Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha –** Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba waalimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze –** Kuna Mstari muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha –** Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu uwepo ili watoto wasichukulie masomo kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka –** Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha –** Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Viunga (links) maalum vya tovuti ya Free Bible Images kwa ajili ya Masomo yote ya daraja zote na mfululizo wote wa Wakati na Biblia yanapatikana kwa barua pepe kutoka kwenye ofisi ya BES. Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kufundisha Mstari Muhimu

1) Mstari unafaa kuandikwa kwenye karatasi au ubaoni na baadhi ya maneno kuondolewa huku watoto wakirudia ule mstari hadi pale maneno yote yatakapoondolewa na watoto kuurudia mstari bila kuangalia maneno.
2) Ili kuwaanzishia watoto Mstari muhimu, mwalimu anaweza kutumia:
   a) Njia ya Hangman yenye vikundi viwili (2 teams) – Unaweza kuwapa watoto baadhi ya nafasi za herufi za ule Mstari muhimu bila herufi zenyewe – Watoto watachagua herufi wanazozitaka mpaka mtu atakapoweza kuuona Mstari muhimu.
   b) Njia ya Sword Drill – watoto wanakuwa na Biblia na wote wanashindana kutafuta mstari huo wa Biblia na atakayeupata wa kwanza ataruhusiwa kuusoma kwa sauti.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
  1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
  2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi10
  3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
  4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0 (Chekechea/Chini ya miaka mitano)<br>Daraja la Kwanza (Miaka mitano hadi saba)<br>Daraja la Pili (Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu (Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne (Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

## A1 Habari ya kwanza
**Mungu aumba ulimwengu – Habari hii inahusu Mungu akiumba mbingu na nchi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu aliiumba dunia.<br>• Tunapaswa kumshukuru Mungu kwa kila kitu ambacho amekiumba.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 1:1***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 1:1-19*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Onesha picha ya nyumba au waambie watoto wachore nyumba zao.<br>• Waulize watoto maswali kuhusu hiyo nyumba – Je, itachukua muda gani kuijenga? Je, utahitaji nini ili kuijenga?<br>• Kujenga nyumba kunagharimu nyenzo nyingi lakini Mungu aliumba ulimwengu bila chochote. |
| **FUNDISHA** | • Hapo mwanzo, Mungu aliziumba mbingu na nchi. Kabla ya Mungu kuumba ulimwengu, kulikuwa na giza tu. ***(Mwanzo 1:1-3)*** – Je, kungekuwa vipi kama ingekuwa giza wakati wote? *(Mchezo wa kufumba macho kwa kutumia kitambaa unaweza kutumiwa kama mfano)*<br>• Siku ya kwanza, Mungu akasema, “Na iwe Nuru.” Mara tu kukawa nuru. Mungu akaita nuru mchana nalo giza akaliita usiku. Badala ya kuwa na giza wakati wote kukawa na nuru. ***(Mwanzo 1:4-5)***<br>• Siku ya pili, Mungu akanena tena na akaumba anga na hewa ambayo ipo duniani kote. Usiku ukaja tena na siku ya pili ikaisha. ***(Mwanzo 1:6-8)*** – *Waambie watoto wavute pumzi kwa kina. Elezea kuwa ni muhimu kuwa na hewa safi kote tunakoishi.*<br>• Hadi wakati huu, dunia ilikuwa imejaa maji na sasa ulikuwa ni wakati wakufanya nchi. Mungu akanena na kufanya mahali kwa ajili ya ile nchi mpya.Yale maji kando mwa nchi yakawa bahari. Kisha Mungu akanena tena na kusema, “Nchi na itoe miche na miti ya kila aina.” Mungu akaangalia vyote alivyoviumba na akasema ni vyema. Hii ilikuwa siku ya tatu. ***(Mwanzo 1:9-13)*** *Waambie watoto wataje baadhi ya mimea inayokua kwenye mazingira yao. Ongelea utofauti kwenye rangi, umbo na ukubwa na pia, ni jinsi gani miche na mimea ni muhimu na yakupendeza.*<br>• Siku ya nne, Mungu akafanya mianga maalum kung’aa angani–Jua kwa ajili ya mchana na mwezi na nyota kwa ajili ya usiku. Mungu akaangalia mianga aliyoiumba na akaona ni vyema. ***(Mwanzo 1:14-19)*** *Zungumza jinsi gani jua ni zuri. Waoneshe ni ajabu gani ya idadi ya nyota!*<br>• *Waelezee watoto kuwa, Mungu aliumba ulimwengu mzuri ambao una kila kitu tunachokihitaji na uwaambie ni muhimu kumshukuru kwa ajili hii.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: tafuta kwenye mtandao wa** FBI – God creates the heavens and the earth |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na kuelezea Mstari muhimu – ***Mwanzo 1:1*** |
| **KUMBUKA** | • Ulimwengu ulikuwa vipi hapo mwanzo?<br>• Nuru ilionekana kwenye siku ya ngapi?<br>• Kwenye siku ya pili, Mungu aliumba anga na _ _ _ _ .<br>• Hapo mwanzo, nchi ilikuwa imejaa nini?<br>• Kwenye siku ya tatu, Mungu aliumba vitu viwili vinavyokua, navyo ni?<br>• Mungu aliumba mwanga upi kwa ajili ya mchana?<br>• Mungu aliumba mwanga upi kwa ajili ya usiku?<br>• Malizia mstari huu – “Hapo mwanzo, Mungu aliziumba ...” |

## A1 Habari ya pili

**Mungu awaumba wanyama na mwanadamu – Habari hii inahusu mwanadamu wa kwanza.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu aliwaumba wanadamu kwa sura yake mwenyewe na wao ni wa muhimu sana kwake.<br>• Inatupasa kuifuata njia ya Mungu kwa sababu alituumba.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 1:31***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 1:20-2:3*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Leta kitu ulichokitengeneza au kukiandaa lakini kikaharibika kwa mfano chapati iliyoungua. Ongea kuhusu jinsi inavyokatisha tamaa pale ambapo mambo hayaendi kama ulivyoyapanga na kutarajia.<br>• Elezea watoto kuwa, Mungu aliumba viumbe vingi tofauti na hakugadhabishwa na chochote alichokiumba.<br>• Au – Watoto wanaweza kuigiza kama wanyama tofauti (fanya iwe na ubunifu na ya kufurahisha kwa mfano uliza watoto wengine jina la mnyama ambaye mmoja wao ameigiza). |
| **FUNDISHA** | • Siku ya tano, Mungu aliumba maelfu na maelfu ya aina tofauti ya ndege na samaki. Mungu akatazama vyote alivyoviumba na akasema “ni vyema”. ***(Mwanzo 1:20-23)*** *Zungumza na watoto kuhusu ndege au samaki wachahe ambao watoto wanawafahamu.*<br>• Siku ya sita, Mungu akaumba wanyama wote. Akamuumba twiga akiwa na shingo ndefu, na simba na chui wakiwa na meno makali. Mungu aliwaumba wote hawa! ***(Mwanzo 1:24-25)***<br>• Ingawa Mungu alikuwa ameumba vitu vingi vizuri, alikuwa bado ana kitu kingine cha kuumba na hiki alikiumba kwa njia maalum zaidi. *Onesha watoto udongo na uwaulize ni nini wangeweza kuumba kwa kuutumia.* Mungu alichukua udongo kutoka kwenye ardhi na akamuumba mwanadamu wa kwanza. Mtu huyu alipata uhai wakati ambapo Mungu alimpulizia pumzi. Mtu huyu wa kwanza aliitwa Adamu. ***(Mwanzo 1:26-31)*** *Elezea watoto kuwa, wakati ambao Mungu alimuumba Adamu, alimuumba kwa mfano Wake mwenyewe (Yaani jinsi alivyo Yeye) kama kielelezo. Hii inamaanisha kuwa, Mungu alimuumba mwanadamu awe kama Yeye kwa baadhi ya mambo. Kwa sababu tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, sisi ni wa tofauti na viumbe wengine na tunaweza kuumba vitu na kuwaza. Inamaanisha pia tunajua tofauti kati ya mema na maovu, na tunaweza kujifunza kumfuata Mungu na Njia Zake.*<br>• Mungu aliumba dunia na vyote vilivyomo kwa siku sita. Alipomaliza, alisema ni vyema. Siku ya saba, alipumzika na kupendezwa na vyote alivyokuwa ameviumba. ***(Mwanzo 2:1-3)*** *Ongelea umuhimu wa kupumzika baada ya kuwa na shughuli nyingi.*<br>• Malizia kwa kusema kuwa, dunia ambayo Mungu alikuwa ameiumba ilikuwa haina kasoro yoyote na Mungu alipendezwa na vyote alivyokuwa ameviumba.<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha:** Power-point- kutoka kwa www.teachingideas.co.uk<br>**Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – God creates the heavens and the earth. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Mwanzo 1:31*** |
| **KUMBUKA** | • Ni siku gani ambayo Mungu aliumba ndege na samaki?<br>• Je, Mungu alisema nini kuhusu ndege na samaki?<br>• Mungu aliumba nini siku ya sita alipoumba wanyama pia?<br>• Mungu alisema nini alipomaliza uumbaji?<br>• Mtu wa kwanza aliitwa nani?<br>• Je, Mungu alitumia nini kumuumba?<br>• Mungu alitumia siku ngapi kuumba ulimwengu na vyote vilivyomo?<br>• Mungu alifanya nini siku ya saba? |

## A1 Habari ya tatu

**Mwanamume na mwanamke wa kwanza – Habari hii inahusu mke wa Adamu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alimuumbia Adamu mke, ambaye alikuwa amsaidie kutunza uumbaji wa Mungu.<br>• Mungu ndiye anayetawala vyote.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 2:18 au Zaburi 24:1***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 2:4-25*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Kama watoto wanaufahamu wa shamba, zungumzia kuhusu mimea ambayo wamewahi kuona shambani au waoneshe maua/matunda/nyasi ambayo inamea kwenye mazingira yao. Kama hawajawahi kuona shamba, waelezee shamba ni nini na jinsi lilivyo.<br>• Elezea kuwa, bustani ya Edeni ilikuwa ya kupendeza sana zaidi ya chochote ambacho tunaweza kuchora au kuwaza.<br>• Jadiliana kuhusu bustani ya Edeni – Je, ungependa kuishi kwenye bustani ya Edeni? Je, ungefurahia nini zaidi ya vyote kwenye ile bustani? Je, unafikiri Adamu angepata upweke kwenye ile bustani? |
| **FUNDISHA** | • Adamu aliishi kwenye bustani nzuri sana iitwayo Edeni. Mungu alimpa Adamu kila kitu ambacho alihitaji kama vile chakula na maji. Mungu pia alimwambia Adamu aitunze ile bustani. ***(Mwanzo 2:15)***<br>• Mungu alimuonesha Adamu viumbe wote wenye uhai aliokuwa amewaumba. ***(Mwanzo 2:19-20)***<br>• Mungu hakutaka Adamu awe mpweke. Adamu alikuwa amezingirwa na wanyama, ndege, miti na mimea mizuri sana lakini Mungu alijua kwamba Adamu alihitaji mtu maalum ambaye wangeishi pamoja kwenye ile bustani. Mungu akamsababishia Adamu usingizi mzito. Alipokuwa usingizini, Mungu akamuumba mwanamke wa kwanza kutoka ubavuni mwa Adamu. Adamu hakuwa peke yake tena, alikuwa sasa na mke aliyeitwa Hawa. Hawa alikuwa rafiki yake alipokuwa akitunza bustani ambayo Mungu alikuwa amemkabidhi. ***(Mwanzo 2:20-24)***<br>• Ile bustani ilikuwa na miti mingi. Katikati ya ile bustani, kulikuwa na mti uitwao “Mti wa ujuzi wa mema na mabaya”. Mungu akawaambia Adamu na Hawa kuwa wangekula kutoka kwenye miti yote kwenye bustani isipokuwa kwenye mti ule wa “Ujuzi wa mema na mabaya”. ***(Mwanzo 2:16-17)*** *Zungumzia kuhusu sheria ambazo watoto wamepewa nyumbani au shuleni. Je, kwa nini tuna sheria? (Ili tuwe salama). Angalia kama watoto wanaelewa sheria au agizo ambalo Mungu alitaka Adamu an Hawa walizingatie.*<br>• *Elezea kuwa Mungu aliumba ulimwengu na sheria au maagizo. Yeye ndiye mwenye uwezo na anayefaa kuwaagiza wanadamu jinsi gani wanapaswa kuishi duniani. Nasi pia, inatupasa kutii sheria au maagizo ya Mungu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – God creates the heavens and the earth. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Mwanzo 2:18 au Zaburi 24:1*** |
| **KUMBUKA** | • Adamu aliishi wapi?<br>• Adamu alitakiwa afanye nini kwenye bustani?<br>• Wanyama walipata majina yao vipi?<br>• Kamilisha sentensi - Mungu alitaka kumuumbia Adamu ________________.<br>• Mungu alitumia nini kumuumba mke wa Adamu?<br>• Mke wa Adamu aliitwa nani?<br>• Taja mti maalum kwenye ile bustani.<br>• Agizo la Mungu kuhusu “Mti wa ujuzi wa mema na mabaya” lilikuwa lipi? |

## A1 Habari ya nne

**Ulimwengu wa Mungu waharibiwa – Habari hii inahusu dhambi ilivyoingia ulimwenguni.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Adamu na Hawa walimwasi Mungu na kuharibu uumbaji wake uliokuwa mkamilifu.<br>• Nasi pia huwa tunamwasi Mungu na inatupasa kutubu dhambi zetu na kumwomba Mungu msamaha.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Warumi 5:12 au Warumi 5:1***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 3:1-24*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Leta picha nzuri kisha iharibu kwa kuichora ovyo ovyo, iharibu uwezavyo.<br>• Jadiliana – Ni nini kilichotokea kwenye ile picha? Je, sasa mwonekano wake uko vipi?<br>• Elezea kuwa, Mungu aliumba ulimwengu uliokuwa mkamilifu lakini ukaharibiwa. |
| **FUNDISHA** | • Wakati ambao ulimwengu uliumbwa, kila kitu kilikuwa kikamilifu hadi wakati ambao adui wa Mungu ambaye ni shetani, kwa mfano wa nyoka, alipokuja kwenye ile bustani. Yule nyoka alizungumza na Hawa na akamshawishi kuwa akila kutoka kwenye ule mti wa "Ujuzi wa Mema na mabaya" atakuwa na ufahamu kama wa Mungu. ***(Mwanzo 3:1-5)***<br>• Hawa akamsikiliza yule adui wa Mungu. Akamwasi Mungu na kula tunda kutoka kwenye ule mti. Akampa Adamu na wakawa wamekula wote wawili. ***(Mwanzo 3:6)***<br>• Jioni hiyo Mungu alitaka kuongea na Adamu na Hawa lakini walikuwa wamejificha kwani walijua kuwa walikuwa wameasi. ***(Mwanzo 3:7-8)*** *Je, umewahi kumwasi mtu? Je, ni nini kilitokea baadaye? Elezea kuwa Adamu na Hawa hawakuweza kujificha ili wasionekane na Mungu na sisi pia hatuwezi kujificha.*<br>• Mungu akawaita, "uko wapi?" alijua kwamba walikuwa wamemwasi. Hata kama alikuwa bado anawapenda, hawakuwa na budi kupata adhabu yao kwa ajili ya kuasi kwao. Mungu akawatoa Adamu na Hawa kwenye bustani ya Edeni. Dhambi zao zilikuwa zimeharibu uumbaji wa Mungu na kuharibu urafiki wao na Mungu. Kwa sababu ya dhambi hiyo ya Adamu na Hawa, michongoma na miiba ilianza kukua. Wanyama na watu wakapata magojwa na la kusikitisha sana, mauti ikaingia duniani. ***(Mwanzo 3:9-24)***<br>• *Mungu pia hafurahi tunapofanya mambo mabaya. Shauriana na watoto ni mambo gani ambayo wao hufanya, ambayo hayampendezi Mungu hata kama anatupenda sana. Mwana wa Mungu alikufa msalabani ili tusamehewe na kuwa marafiki wa Mungu tunapo mwamini.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Adam and Eve disobey God. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Warumi 5:12 au Warumi 5:1*** |
| **KUMBUKA** | • Ni nani aliyemshawishi Hawa ale lile tunda?<br>• Je, shetani alimshawishi Hawa kula tunda kwa njia gani?<br>• Hawa alimpa nani lile tunda?<br>• Adamu na Hawa walifanya nini Mungu alipowaita?<br>• Je, Mungu alijihisi vipi kwa ajili ya lile jambo ambalo Adamu na Hawa walikuwa wamelitenda?<br>• Je, ni nini kilichotokea kwa Adamu na Hawa?<br>• Je, Mungu anajihisi vipi tunapotenda mambo mabaya?<br>• Je, tunasamehewa vipi kwa makosa ambayo tumetenda? |

## A2 Habari ya kwanza

**Nuhu amtii Mungu – Habari hii inahusu Nuhu akijenga safina.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Nuhu na familia yake na wanyama waliokuwepo ndani ya safina walikuwa salama wakati wa gharika.<br>• Kwa hiyo Mungu ametupa njia ya sisi pia kuokolewa, kwa hiyo tunaweza kumuuamini kama Nuhu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 16:31***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 6:5-22*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Wape watoto fursa ya kukuambia wanyama wanaowapenda zaidi.<br>• Jadiliana nao jinsi hali ingekuwa kama wanyama wote hawa wangekuwa kwenye sehemu moja! Je, ni sehemu gani wangetoshea wanyama wote? Je, sehemu hiyo ingekuwa na hali gani? Ingekuwa na harufu gani?<br>• Elezea kuwa wanaenda kujifunza kuhusu habari kwenye Biblia ambapo watu kadhaa na wanyama wengi waliingia kwenye aina ya meli kubwa. |
| **FUNDISHA** | • Wakati ambapo Mungu aliumba ulimwengu wetu, kila kitu kilikuwa kinapendeza na kizuri. Baada ya muda mfupi, Adamu na Hawa walimuasi. Wana wao wakawa wabinafsi na wenye uovu na Mungu akajuta kwa nini aliwaumba. ***(Mwanzo 6:5-6)***<br>• Dunia yote ilikuwa imejaa uovu lakini kuna mtu mmoja aliyempendeza Mungu sana! Mtu huyu aliitwa Nuhu. Yeye na mke wake pamoja na wana wao watatu na wake zao walijitahidi kufanya mambo kama alivyotaka Mungu. Watu wa jamaa zao na wengine walioishi karibu nao walipenda kujifurahisha na wakamsahau Mungu kabisa. ***(Mwanzo 6:8-10)***<br>• Mungu akaona kuwa dunia ilikuwa imeharibika na akaamua kuiadhibu. Alimuuomba Nuhu ajenge aina kubwa ya meli iitwayo safina. Ilipokamilika, Mungu aliruhusu gharika ya ajabu juu ya nchi. Kila chenye uhai kilikufa lakini Nuhu na familia yake walikuwa salama kwenye safina. ***(Mwanzo 6:13-18)***<br>• Nuhu alifanya kila kitu kama alivyoagizwa na Mungu. Inawezekana alitumia muda mrefu kutengeneza ile meli kubwa au safina. Labda muda wa miaka mia moja! *Zungumzia kuhusu ukubwa wake, kubwa kama uwanja wa mpira na ndefu kama jengo la ghorofa tatu.* Mwishowe, safina ilikamilika lakini baada ya kazi nyingi. ***(Mwanzo 6:22)***<br>• Mungu akamwambia Nuhu awalete wanyama na ndege wa aina zote na kuwaingiza ndani ya safina. *Taja baadhi ya wanyama ambao watoto walikuwa wamewataja mwanzoni mwa somo hili.* Walikuwa salama pamoja na familia ya Nuhu.Wataje wale watu wanane wa familia ya Nuhu walioingia kwenye safina. *Wakati ambao wote waliingia, Mungu aliufunga ule mlango wa safina.* Mpango wake wakuwaokoa ulikuwa umekamilika. ***(Mwanzo 7:13-16)***<br>• *Elezea kuwa, nasi pia tumefanya mambo kwa njia ambayo siyo sahihi. Tunahitaji kuokolewa na kusamehewa ili tusipate adhabu ya dhambi zetu. Mungu ametupa njia ya kuwa salama tunapomwamini Mwana wake ambaye ndiye Bwana Yesu. Yeye ni kama safina ambayo Mungu ametupa.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Noah and the Ark. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee ule Mstari muhimu – ***Matendo 16:31*** |
| **KUMBUKA** | • Nini lilikuwa tatizo duniani?<br>• Mungu aliamua kufanya nini?<br>• Ni nani aliyemfurahisha Mungu?<br>• Mungu alimuagiza Nuhu kufanya nini?<br>• Ni nani aliyeingia ndani ya safina?<br>• Ni nani aliyefunga mlango wa safina?<br>• Kwa nini wale watu ndani ya safina walikuwa salama?<br>• Sisi tunawezaje kuwa salama na kuepuka adhabu ya dhambi zetu? |

## A2 Habari ya pili

**Salama ndani ya safina – Habari hii inahusu wakati ambao gharika ilianza.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Nuhu na familia yake walikuwa salama kwa sababu walimtii na kumwamini Mungu.<br>• Mungu ameahidi kutuweka salama tunapomwamini.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mithali 29:25***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 7:1-16*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waambie watoto waelezee kuhusu kitu ambacho walikigenga au kukitengeneza – Je, ulitumia nini kukijenga?Je , ilikuwa kazi ngumu? Je, kuna mtu aliyekusaidia?<br>• Elezea kuhusu ile habari ya Nuhu tuliyojifunza kwenye HABARI YA KWANZA – Je, Nuhu alitumia nini kuijenga safina? Je, unafikiri ilikuwa ni kazi ngumu? Kwa nini aliijenga?<br>• Sisitiza kuwa, hata kama ilikuwa ni kazi ngumu, Nuhu aliijenga ile safina kwa sababu Mungu alikuwa amemwagiza kufanya hivyo. Aliyatii maagizo ya Mungu kikamilifu. |
| **FUNDISHA** | • Sasa, Nuhu na familia yake walikuwa salama kwenye safina. ***(Mwanzo 7:6-7)***<br>• Baada ya siku saba, mvua ikaanza kunyesha. Ikanyesha siku baada ya siku! Nyasi zote na maua yakafunikwa na maji . Mito na bahari ikawa ni gharika kubwa. ***(Mwanzo 7:17-20)***. *Elezea kuwa, wale watu waliokuwa wamemcheka Nuhu walikuwa nje ya safina na hawangeweza kuingia mle.*<br>• Maji yakaendelea kuwa mengi. Yakafunika majengo, miti na pia milima iliyokuwa mirefu sana. ***(Mwanzo 7:20-21)*** *Jaribu kuwaza ni jinsi gani Nuhu na familia yake walijihisi mle ndani ya safina? Je, ni nini kingetokea kama Nuhu asingemtii Mungu?*<br>• Nuhu, familia yake na wanyama wote waliokuwa ndani ya safina walikuwa salama! Kwa sababu Nuhu alikuwa amemwamini na kumtii Mungu, alifanya wote hao kuwa salama. ***(Mwanzo 7:23)***<br>• *Elezea watoto kuwa, Mungu anataka nasi tumtii na kumwamini. Mungu ameahidi kutuweka salama pia, tukimwamini na kumtii kama Nuhu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Noah and the Ark. Pia picha za bure zinapatikana kwenye www.bibleforchildren.org |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee ule Mstari muhimu – ***Mithali 29:25*** |
| **KUMBUKA** | • Je, Nuhu alionesha vipi kuwa alimwamini Mungu?<br>• Je, ni nani aliyeingia kwenye safina pamoja na Nuhu?<br>• Je, walikuwa ndani ya safina kwa muda gani kabla mvua haijaanza kunyesha?<br>• Je, maji yalienda juu kiasi gani?<br>• Je, ni nani aliyekuwa salama?<br>• Je, kwa nini Nuhu aliwekwa salama?<br>• Je, ni nani atatuweka salama tukimwamini? |

<u>A2 Habari ya tatu</u>

**Mwanzo mpya – Habari hii inahusu wakati ambao gharika ilipoisha.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu aliwapa Nuhu na familia yake nchi mpya na safi ya wao kuishi.<br>• Mungu anaweza kufanya maisha yetu yawe safi na mpya tunapomwomba msamaha.<br><br>**Mstari muhimu:** ***2 Wakorintho 5:17***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 8:1-19*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Elezea watoto kuwa, Nuhu pamoja na familia yake walikaa kwenye safina kwa muda mrefu.<br>• Wape watoto muda wa kuwaza hali ilivyokuwa ndani ya safina – Je wangefanya nini siku nzima mle ndani? Je, wangejihisi vipi mle ndani? |
| **FUNDISHA** | • Baada ya siku arobaini, mvua ikaacha kunyesha. Lakini yale maji ya gharika yalifunika milima. ***(Mwanzo 8:1-4)***<br>• Siku moja, Nuhu akamtoa kunguru nje ya safina ili kuangalia kama maji yalikuwa yamepungua juu ya nchi. Lakini kunguru hakumrudia. Baadaye, Nuhu akamtoa njiwa, naye akamrudia. Baada ya wiki moja, akamtoa tena yule njiwa. Kila mtu alifurahi sana aliporudi akiwa na jani la mzeituni kinywani mwake. *Elezea kuwa, hii ilimaanisha kuwa, miti sasa ilikuwa inaonekana juu ya maji.* ***(Mwanzo 8:6-11)***<br>• Baada ya siku zingine saba, Nuhu akamtoa tena yule njiwa. Lakini, hakurudi tena. Nuhu alijua kuwa, maji yalikuwa yamepungua zaidi na yule njiwa alikuwa amepata makao mapya kule nje ya safina. Mwishowe, ile safina ikatua juu ya milima mirefu ya Ararati. ***(Mwanzo 8:4)***<br>• Wakati ambao nchi ilikauka, Mungu akamwambia Nuhu atoke nje ya safina pamoja na wanyama waliokuwamo mle ndani. Je, ilikuwa ni habari nzuri ya jinsi gani kwa kila mtu! Walikuwa mle ndani ya safina kwa muda mrefu sana! *Je, unafikiria Nuhu pamoja na familia yake walijihisi vipi walipotoka nje ya safina? Jadiliana na watoto kuhusu mwonekano wa nchi ile mpya.* ***(Mwanzo 8:15-19)***<br>• *Elezea watoto kuwa, nasi hatuna tofauti na wale watu wa siku hizo za Nuhu. Mungu anaweza kutuondolea mambo mabaya maishani mwetu pia na kutupa mioyo mipya na safi. Inatupasa kumwomba Mungu msamaha na kumwamini Bwana Yesu aliyekufa msalabani na kutuondolea dhambi.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Noah and the Ark.<br>Pia picha za bure zinapatikana kwenye www.bibleforchildren.org |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***2 Wakorintho 5:17*** *ukielezea kuwa Bwana Yesu anaweza kubadilisha maisha yetu kutoka ndani.* |
| **KUMBUKA** | • Ni ndege yupi wa kwanza ambaye Nuhu alimtoa nje ya safina?<br>• Je, njiwa alileta nini kinywani mwake mara ya pili?<br>• Je, safina ilitua wapi?<br>• Ni nani aliyemwambia Nuhu atoke nje ya safina?<br>• Ni nani aliyeokolewa kutokana na gharika?<br>• Je, ni nani aliyeadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu?<br>• Je, inatupasa kufanya nini ili kuwa na moyo safi?<br>• Jaza neno lililokosekana: “Mtu akiwa ndani aya Kristo, amekuwa ...................kipya.” |

## A2 Habari ya nne

## Ahadi za Mungu – Ahadi hii inahusu shukrani za Nuhu.

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Kila mara, Mungu huheshimu ahadi zake.<br>• Kama vile Mungu alivyomlinda Nuhu na familia yake, ameahidi kuwa, hatawaacha kamwe wale wamwaminio na kumfuata.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 13:5***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 8:20-22 au 9:7-17*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Elezea watoto mfano wako mwenyewe kuhusu wakati ambao umewahi kupewa ahadi na mtu.<br>• Mpe kila mtoto fursa ya kumwambia mwezake kuhusu wakati ambao alipewa ahadi na mtu.<br>• Waulize watoto kama kuna mtu amewahi kuvunja ahadi aliyokuwa amewapa.<br>• Waambie watoto kuwa, Biblia imejaa ahadi za Mungu naye kamwe havunji ahadi zake.<br>• Waambie watoto kuwa, tukichagua kumwamini na kumfuata Mungu, Yeye ameahidi kuwa hatatuacha. |
| **FUNDISHA** | • Nuhu na familia yake walikuwa salama!  Walikaa kwenye safina kwa muda mrefu. Mungu akamwambia Nuhu na familia yake pamoja na wanyama watoke nje ya safina. ***(Mwanzo 8:15-19)***<br>• Kitu cha kwanza ambacho Nuhu alitaka kukifanya ni kumshukuru Mungu kwa kuwalinda yeye na familia yake kutokana na ile gharika! Alifanya hivi kwa kukusanya mawe na kuyapanga ili kujenga madhabahu. Siku zile za Nuhu, watu walijenga madhabahu na kutoa sadaka za kuteketeza mbele za Mungu. Walifanya hivi ili kumshukuru kwa yote aliyokuwa amewatendea. ***(Mwanzo 8:20-21)*** *Je, ni mambo ya aina gani ambayo tunaweza kumshukuru Mungu kwayo? (Unaweza kuandika orodha ya vitu vya kumshukuru Mungu kwenye ubao au karatasi kubwa)*<br>• Mungu alifurahi sana kwa sababu Nuhu na familia yake walikumbuka kumshukuru. Baadaye aliwapa ahadi nzuri sana, aliwaambia “sita ilaani nchi tena kwa gharika”. ***(Mwanzo 8:21-22)***<br>• Kisha Mungu akawaonesha kitu ambacho kilikuwa ni ishara ya kuwakumbusha ahadi yake. Ilikuwa ni upinde wa mvua. Kila mara Nuhu na familia yake walipouona upinde wa mvua, walikumbuka ahadi ya Mungu. ***(Mwanzo 9:12-13)*** *Zungumzia upinde na rangi zake za kupendeza. Watie moyo watoto wakumbuke Mungu na ahadi yake wakati mwingine wakiona upinde wa mvua.*<br>• *Je, Mungu aliiheshimu ahadi yake aliyompa Nuhu? Wasaidie watoto kuelewa kuwa, Mungu bado anaheshimu ahadi yake ya kuwa nasi tunapomwamini. (Angalia Mstari muhimu wa pili)*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Noah and the Ark. Pia picha za bure zinapatikana kwenye www.bibleforchildren.org |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Waebrania 13:5*** |
| **KUMBUKA** | • Chagua baadhi ya maswali kwenye masomo ya hapo awali ya Nuhu ili kuona kama watoto wanakumbuka habari hiyo ya Nuhu.<br>• Rudia Mistari Muhimu ambayo watoto walijifunza walipokuwa wanasoma habari ya Nuhu.<br>• Watoto wanaweza kuchora picha ya sehemu ya habari waliyoipenda zaidi au kuandika sentensi kuhusu walichojifunza.<br>• Kwenye vikundi, watoto wanaweza kutengeneza picha za watu na wanyama wakitoka kwenye safina, madhabahu na pia upinde wa mvua. |

<u>**A3 Habari ya kwanza**</u>

**Yesu akamwita Petro – Habari hii inahusu kumfuata Bwana Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alihitaji wasaidizi wakutenda kazi pamoja naye na pia wangeendeleza kazi hiyo siku zijazo.<br>• Ili kuwa msaidizi wake, lazima tumfuate Yesu na kumtii.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mathayo 4:19***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 4:18-22*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Zungumzia kuhusu marafiki. Waulize watoto walikutana wapi na marafiki wao kwa mara ya kwanza? Kwa nini ni jambo zuri kuwa na marafiki? Je, ni vizuri kuwa na marafiki wa aina gani? (Mapendekezo yanaweza kuwa mkarimu, anayeweza kusaidia, anayeaminika.....)<br>• Elezea kuwa, Bwana Yesu pia alikuwa na marafiki wazuri na wanaenda kujifunza kuhusa baadhi yao.<br>• Andaa mazingira – ziwa kubwa la Galilaya ambalo limezungukwa na milima. Wavuvi walikuwa hapa wakivua samaki. Elezea ni jinsi gani wangevua samaki (wakiwa na mashua, nyavu, na kadhalika). Haikuwa rahisi! |
| **FUNDISHA** | • Yesu akamwita Petro na kaka yake Andrea. ***(Mathayo 4:18-19)*** Petro na Yohana walikuwa wamekutana na Bwana Yesu hapo awali na walikuwa wametambua jinsi gani alikuwa wa muhimu. Sasa Yesu aliwataka kuacha uvuvi na kumfuata ili kumsaidia kwenye kazi yake! *Tumia maneno haswa ambayo Yesu aliyatumia na uelezee kuwa, kazi yao mpya ilikuwa ni kuwaleta watu wengine ili wamjue Yesu. Ilikuwa ni kazi maalum sana ambayo Yesu alikuwa amewaomba kufanya!*<br>• Majibu ya Petro na Andrea. ***(Mathayo 4:20)*** Walijua mara moja kuwa hilo lilikuwa ni jambo nzuri la kufanya. Walionesha utayari wao kwa kumfuata Yesu mara moja. *Linganisha tukio hili na tukio kwenye maisha ya watoto ambapo wanatii mara moja. Jaribu kuwaza kuhusu hisia za Petro na Andrea wakati (walikuwa na msisimko, furaha na kujihisi watu maalum kwa sababu Yesu alikuwa amewachagua) Kwa watoto wa Daraja la pili, elezea kuwa, Petro na Andrea walikuwa sasa ni wanafunzi wa Yesu . Hii inamaanisha kwamba, walikuwa tayari kumfuata popote aendapo, kujifunza kutoka kwake na kumtii.*<br>• Yesu anawaita Yakobo na Yohana. ***(Mathayo 4:21, 22)*** Baadaye siku hiyo, Yesu akawaita wavuvi wengine wawili na wao pia wakamfuata Yesu. (Daraja la pili)<br>• *Bwana Yesu anataka kila mmoja wetu awe mfuasi wake. Tukiwa wafuasi wake, atatutumia kwa kazi yake. Kama wale wavuvi kwenye Biblia, inatupasa kutii Neno Lake. Je, tunapata wapi Neno Lake? ( Taja umuhimu wa Biblia)*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Jesus calls His first disciples. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari muhimu, angalia kama wameelewa “wavuvi wa watu” – ***Mathayo 4:19*** |
| **KUMBUKA** | • Je, kwa ujumla Yesu aliwaita wanafunzi wangapi?<br>• Je, walifanya kazi wapi?<br>• Kaka yake na Andrea aliitwa nani?<br>• Je, Yesu aliahidi kuwa wale waliomfuata wangekuwa kina nani?<br>• Je, Petro na Andrea waliacha nini walipomfuata Yesu?<br>• Je, Petro na Andrea walifanya nini ili kuonesha kuwa walikuwa makini kuwa wanafunzi wa Yesu?<br>• Je, wale ndugu wawili ambao Yesu aliwapata baada ya Petro na Andrea walikuwa akina nani?<br>• Je, Yakobo na Yohana walikuwa wanafanya nini wakati ambao Yesu aliwajia?<br>• Je, ni nani aliyekuwa kwenye chombo pamoja nao?<br>• Kamilisha sentensi hii – Ukitaka kuwa mfuasi wa Yesu, lazima .............. Neno Lake. |

## A3 Habari ya pili
## Yesu amsaidia Petro – Habari hii inahusu Petro alivyojitambua kuwa mwenye dhambi

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Nguvu za Yesu zilikuwa na mguso kwenye maisha ya Petro.<br>• Yesu ni Mwana wa Mungu na anataka tumfuate kama vile Petro alivyomfuata.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Luka 5:10***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Luka 5:1-11*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waombe watoto watafakari mambo ambayo wanayafanya vizuri zaidi. Wakumbushe watoto kuwa, nao wana ujuzi na uwezo.<br>• Petro alikuwa vizuri kwenye uvuvi. Alikuwa mvuvi kwa muda mrefu. Lakini kwenye habari ya leo, Petro alijifunza kuwa, ilimpasa kutii maelekezo ya Yesu ili kufanikiwa! (Inakupasa kuelezea kuwa, wakati mwingine Petro anaitwa Simoni au Simoni Petro) |
| **FUNDISHA** | • Wakumbushe watoto kuhusu mazingiza ya somo la kwanza ambalo umelimaliza kabla ya hili. Yesu alitumia chombo cha Petro na kuwafundisha watu habari za Mungu. ***(Luka 5:1-3)***<br>• Amri ya Yesu kwa Petro.Yesu akamwambia Petro, waende kwenye vilindi vya maji, washushe nyavu zao na kuvua samaki. ***(Luka 5:4-5)*** *Jaribu kuwaza kuhusu hisia za Petro kuhusu jambo hili.*<br>• Uvuvi wa samaki wengi. ***(Luka 5:6, 7)*** *Ulileta utofauti na uvuvi wa usiku uliokuwa umepita na pia samaki waliowapata.* Huu ulikuwa ni muujiza! Muumbaji wa samaki alikuwa pale pamoja na Petro kwenye chombo na ilikuwa ni nguvu yake iliyowaleta samaki kwenye nyavu za Petro.<br>• Majibu ya Petro ***(Luka 5:8, 9)*** Elezea kuwa, Petro aligundua kwa njia mpya Yesu alikuwa ni nani. Hakuwa mtu wa kawaida kama Petro. Alikuwa Bwana Yesu mwenye nguvu zote na kwa kujilinganisha naye, Petro alijua kuwa, yeye alikuwa mwenye dhambi.<br>• Kazi mpya ya Petro ***(Luka 5:10)*** Yesu akamwambia Petro kuwa, Kutoka wakati ule, atakuwa mvuvi wa watu! *Hakikisha kuwa watoto wanaelewa jambo hili ambalo lilikuwa pia kwenye somo la kwanza.* Petro aligundua kuwa, Bwana Yesu alikuwa na jambo la muhimu zaidi ambalo alitaka afanye kwa hiyo akaacha kila kitu na kumfuata Yesu. ***(Luka 5:11)***<br>• *Bwana Yesu anataka tutambue ukuu na nguvu zake. Tunaweza kuwa naye maishani mwetu. Je, ni mabadiliko ya aina gani ambayo atafanya maishani mwetu tunapoamua kumtii na kumfuata kama Petro?*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Jesus and the Fishermen. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Luka 5:10*** |
| **KUMBUKA** | • Je, Yesu alitumia nini kilichokuwa ni cha Petro?<br>• Je, Yesu alimuomba Petro kufanya nini baada ya kumaliza kuwafundisha makutano?<br>• Je, lini mara ya mwisho Petro alikuwa amevua samaki?<br>• Je, Petro alichukulia vipi ule uvuvi wa samaki wengi?<br>• Tendo maalum ambalo Yesu anaweza kufanya kwa sababu ni Mwana wa Mungu linaitwa nini?<br>• Kwa nini Petro alianguka magotini pa Yesu?<br>• Ni nani mwingine alishangazwa na ule uvuvi wa samaki wengi?<br>• Je, Yesu alimwambia Petro angefanya nini kuanzia wakati ule?<br>• Je, Petro na rafiki zake walifanya nini mwisho wa habari hii?<br><br>**Onesha:** Kama unafundisha kwenye mazingira ya shule, au mahali ambapo kuna penseli, karatasi na mkasi, kila mtoto anaweza kuchora samaki mmoja na kumkata. Samaki wote wanaweza kuinuliwa kwa pamoja au kupangwa pamoja na maneno kuandikwa ili kuwakumbusha watoto kuhusu habari hii. Kwa mfano, Bwana Yesu alimsaidia Petro kuvua samaki wengi. |

<u>**A3 Habari ya tatu**</u>

**Yesu atuliza dhoruba – Habari hii inahusu nguvu za Bwana Yesu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu aliweza kutuliza dhoruba kwa sababu ni Mwana wa Mungu.<br>• Tunapaswa kumwamini Bwana Yesu kama Mwana wa Mungu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mathayo 8:27***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 8:23-27*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Elezea kuhusu hali ya hewa ambayo watoto watafahamu kwa urahisi. Je, hali ya hewa hubadilika kwa ghafla? Kwa mfano, mvua kubwa kunyesha kwa ghafla?<br>• Elezea ni jinsi gani hali ya hewa huathiri safari ya meli na pia athari ya mawimbi. Kwenye habari ya leo, Yesu na wanafunzi wake walikuwa wanasafiri kwa meli (mashua) kwenye bahari ya Galilaya. |
| **FUNDISHA** | • Mwanzo ulio tulia. Elezea hali ya utulivu. Baada ya muda mfupi, Yesu akalala. ***(Mathayo 8:23, 24)***<br>• Mawimbi. Kwa ghafla, kukawa na mawimbi ya kutisha na wanafunzi wakaanza kuogopa. ***(Mathayo 8:24)*** Elezea hilo tukio kwa kusisimua na kwa uwazi – ile kelele, yale mawimbi yakifunika chombo, jitihada za kutoa maji kwenye chombo...<br>• Woga/ hofu ya wanafunzi. *Elezea kuwa waliogopa kwa sababu walifikiri wangezama. Kwa haraka, wakaenda kumwamsha Yesu ili awaokoe.* Tumia maneno hasa waliyoyatumia. ***(Mathayo 8:25)*** Yesu alighadhabika kwa sababu wanafunzi walikuwa bado hawajamwamini. *Elezea kuwa, kuwa na imani ni kumtegemea.* ***(Mathayo 8:26a)***<br>• Nguvu za Yesu. Yesu akatuliza mawimbi. ***(Mathayo 8:26b)*** Angalia **Marko 4:39** *Sisitiza kuwa, mawimbi yalitulia kabisa papo hapo!*<br>• Kustaajabu kwa wanafunzi ***(Mathayo 8:27)*** *Elezea kuwa, walipoona nguvu za Yesu juu ya upepo na mawimbi, waligundua kwamba, alikuwa mkuu zaidi yao.*<br>• *Hakikisha kuwa watoto wanaelewa kwa nini Yesu aliweza kutuliza mawimbi. Yeye ni Mwana wa Mungu aliyeumba yote.*<br>• *Ana nguvu juu ya kila kitu ulimwenguni hata hali ya hela. Wahamasishe watoto wafikiri kuhusu hali katika maisha yao walipomwamini Yesu na kugundua kwamba Yeye huwa anatawala yote.*<br>• *Tunahitaji kuamini kuwa, Yeye ni Mwana wa Mungu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Jesus calms the storm. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Mathayo 8:27*** |
| **KUMBUKA** | • Mambo haya yalitendeka wapi?<br>• Ni nani aliyepanda kwenye chombo wa kwanza?<br>• Je, mawimbi yalifanya nini dhoruba ilipoanza?<br>• Je, Yesu alikuwa anafanya nini dhoruba ilipoanza?<br>• Kwa nini wanafunzi walimwamsha Yesu?<br>• Kwa nini Yesu aligadhabishwa nao?<br>• Ni vitu gani viwili ambavyo Yesu alivituliza?<br>• Je, Mstari muhimu unapatikana wapi?<br>• Kwa nini Yesu alituliza mawimbi lakini hakuna mwanafunzi wake aliyeweza kufanya hivyo?<br>• Kitu kizuri alichokifanya Yesu kinaitwa nini?<br><br>**Igiza:** Habari hii inaweza kuwa igizo zuri sana kukiwa na wanafunzi kumi na wawili kwenye chombo. Wengine wanaweza kufanya ile sauti ya dhoruba. Mwalimu anaweza kusoma habari hii halafu watoto kwa ubunifu wafanye matendo na kuweza kusema baadhi ya maneno kwa usahihi. |

# A3 Habari ya nne

## Yesu amwokoa Petro – Habari hii inahusu sala fupi ya Petro.

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alimwokoa Petro kwa kujibu sala yake fupi.<br>• Inatupasa kumwamini Bwana Yesu ili tuokolewe.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mathayo 14:33***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 14:22-33*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Elezea kuwa, ukikaa na mtu kwa muda mrefu, utamjua yule mtu zaidi. Unaweza kuwasaidia watoto kukumbuka ni mambo gani ambayo Petro alikuwa amejifunza kuhusu Yesu hadi wakati huu.<br>• Wape watoto fursa ya kusema mawazo yao na kama una ubao au sehemu ya kuandika, yaandike. Kwa mfano, Yesu ndiye Mwana wa Mungu, anaweza kutenda miujiza, ana nguvu juu ya bahari.<br>• Kwenye habari ya leo, Petro anajifunza zaidi kumhusu Yesu. |
| **FUNDISHA** | • Wanafunzi walikuwa chomboni na kutangulia mbele, naye Yesu akaenda kuomba peke yake. ***(Mathayo 14:22-23)*** *Elezea umuhimu wa maombi kwenye maisha ya Yesu.*<br>• Mawimbi. ***(Mathayo 14:24)*** *Kumbuka mawimbi au dhoruba kwenye habari ya wiki iliyopita na uelezee mawimbi haya.* Yesu aliona kuwa wanafunzi walikuwa kwenye shida na akatembea juu ya maji akiwaelekea usiku wa manane. ***(Mathayo 14:25-27)*** *Elezea jinsi wanafunzi walihisi na kuwaza. Kumbuka maneno ya Yesu ya kuwafariji.*<br>• Ombi la Petro. Petro alikuwa anataka kuhakikisha kama Yule alikuwa ni Yesu. Kwa Hiyo akamwambia kama ni yeye, amwambie atembee juu ya maji! Yesu akamwambia, “Njoo”. Petro akashuka kwenye chombo na akaanza kutembea kwa miguu juu ya maji akimwelekea Yesu. ***(Mathayo 14:28-29)*** Kila kitu kilikuwa sawa hadi wakati ambao Petro aliacha kumwangalia Yesu na akaangalia mawimbi. Hapo hapo, akaanza kuzama!<br>• Yesu akamwokoa Petro. *Tumia maneno ya Petro kueleza jinsi gani kwa haraka alimlilia Yesu amwokoe.* ***(Mathayo 14:30-32)*** Baadaye, wote wakaingia kwenye chombo na upepo ukatulia. *Elezea mtazamo wa wanafunzi baada ya tukio hili.* ***(Mathayo 14:35)***<br>• *Petro alihitaji kuokolewa ili asizame. Nasi tunahitaji kuokolewa kutoka kwenye dhambi maishani mwetu. Ni Yesu tu anayeweza kutufanyia hivi.Yesu alichukua adhabu ya dhambi zetu alipokufa msalabani. Inatupasa kumwamini.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Jesus walks on the water. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Mathayo 14:33***<br>*Elezea kuabudiwa kunamaanisha nini. Wafunzi walishangaa na wakajawa na furaha kwa sababu ya yale waliokuwa wamejua kuhusu Yesu. Elezea kuwa huu ni usemi mzuri kwa kila mtu, mahali popote anayempenda Bwana Yesu, anastahili kusema kutoka moyoni mwake.* |
| **KUMBUKA** | Maswali yanaweza kutoka kwenye habari zote za somo la A3. Kama una kadi, unaweza kuchora samaki wa ukubwa tofauti. Kwa kujibu swali, wanafunzi wanaweza kuchagua samaki kutoka kwa zile kadi hapo mbele. Kila samaki atakuwa na pointi zilizoandikwa juu yake.Kuwa na vikundi viwili kisha ujumlishe pointi za kila kikundi.<br><br>• Je, habari hizi zote zilitokea wapi?<br>• Kamilisha mstari: “Njoo nifuate nami nita …….”<br>• Je, Yesu alimwambia nani maneno haya?<br>• Je, Petro alifanya nini alipoona wamevua samaki wengi?<br>• Kamilisha mstari huu, “Huyu ni mtu wa namna gani ……”<br>• Kwa nini Bwana Yesu alienda mlimani?<br>• Kitu gani kiliwafanya wanafunzi kuwa na hofu?<br>• Je, Petro alijifunza nini kuhusu Yesu kwenye habari hii? |

## A4 Habari ya kwanza

**Petro alala usingizi – Habari hii inahusu Bwana Yesu akiomba kwa Baba Yake.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Maombi yalikuwa muhimu kwa maisha ya Bwana Yesu<br>• Ni muhimu kuomba.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Yohana 15:14***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 26:36-46*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Ongea kuhusu vitu ambavyo watoto wanaona sio rahisi kufanya, kwa mfano, kukimbia sehemu ya mwisho kwenye mashindano ya kukimbia mbio za muda mrefu, kusikiliza na kuwa makini kwa muda mrefu, kukaa macho kwenye sherehe za usiku.<br>• Kwenye habari ya leo, Yesu anahitaji msaada maalum kutoka kwa rafiki yake Petro. Tuangalie kama Petro aliweza kufanya kile ambacho Yesu alimwomba kufanya! |
| **FUNDISHA** | • *Toa maelezo ya habari hii.* Yesu alijua kuwa baada ya muda mfupi, wakati utawadia ambao atakufa msalabani. Alikuwa ameshapata chakula cha mwisho pamoja nao. Kila mara, Yesu alimwomba Baba yake na alijua umuhimu wakuomba wakati huu kwa ajili ya yaliyokuwa mbele yake. Akawapeleka wanafunzi wake kwenye bustani ambayo alikuwa akienda kuomba mara kwa mara. Usiku huu, alitaka rafiki zake watatu wawe naye kwenye maombi. Walikuwa ni Petro, Yakobo na Yohana.<br>• Yesu akawaambia Petro, Yakobo na Yohana wakeshe na kuomba. ***(Mathayo 26:36-37)*** Kisha Yesu akaondoka akaenda kumwomba Baba yake. *Elezea jinsi gani Yesu alihisi wakati huo. Maombi yake yalionesha kuwa alitaka kumfurahisha Baba yake kwa kila kitu.* ***(Mathayo 26:38-39)*** Baada ya saa moja, Yesu akarudi na kuwakuta Petro na wanafunzi wengine wamelala. *Ongea kuhusu jinsi gani hakufurahishwa na jambo hili.* ***(Mathayo 26:40-41)***<br>• Yesu akaenda kuomba kwa mara ya pili na aliporudi tena, akawakuta rafiki zake wamelala. ***(Mathayo 26:42-43)***<br>• Yesu akaenda kuomba na kwa mara ya tatu aliporudi, akawakuta wamelala. *Elezea jinsi gani Petro na wenzake walikuwa wamemkosea Yesu. Wote walikuwa wameshindwa kuomba kwenye wakati huu mgumu ambao walihitaji kuomba sana.* ***(Mathayo 26:44-45)***<br>• Wakati huo, adui wa Yesu wakaja na kumkamata. ***(Mathayo 26:45b-46)***<br>• *Kwa kumalizia, elezea umuhimu wa maombi kwetu sisi. Maombi yanatusaidia kupata nguvu kutoka kwa Mungu na kushinda majaribu.Toa baadhi ya mifano ambayo watoto wanaweza kuelewa.*<br>• *Petro na wengine walishindwa kutii amri ya Yesu ya "kukesha na kuomba" lakini Yesu anataka sisi tutii amri zake.*<br>• *Kinyume na wale wanafunzi, Yesu kamwe hakutuacha. Aliendelea kuomba na akapata nguvu ya kwenda msalabani na kuyatoa maisha yake kwa ajili yetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Jesus prays in the Garden of Gethsemane. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Yohana 15:14***. *Wasaidie watoto kuelewa kuwa, ni fursa ya kipekee kuhesabiwa kama rafiki wa Yesu.* |
| **KUMBUKA** | • Je, Yesu alienda kuomba wapi?<br>• Ni wanafunzi gani aliotaka wakeshe na kuomba pamoja naye?<br>• Je, Yesu alikuwa anaombea nini?<br>• Je, Yesu alijihisi vipi alipokuwa anaendelea kuomba?<br>• Je, Yesu aliomba kwa muda gani mara ya kwanza?<br>• Kwa nini wanafunzi walishidwa kuomba?<br>• Yesu aliwaambia waombe mara ngapi?<br>• Je, nini kilitokea baada ya Yesu kumaliza kuomba?<br>• Je, Mstari muhimu unapatikana wapi?<br>• Je, Yesu anatuita jina lipi tukimtii? |

## A4 Habari ya pili

**Petro afanya mapigano – Habari hii inahusu kilichotokea Yesu alipokamatwa.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Yesu alikubali kukamatwa na kuuwawa kwa ajili yetu.<br>• Inawezekana kukabiliana vizuri na hasira kwenye wakati mgumu maishani.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Waefeso 4:26***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 26:47-56*** |
| **TOA UTANGULIZI** | Angalia habari iliyopita kuhusu kilichotokea kwenye bustani. Petro na rafiki zake hawakuomba kama alivyowaambia Yesu. Sasa, kulikuwa na changamoto za kukumbana nazo. Je, iliwapasa kufanya nini? |
| **FUNDISHA** | • Andaa mandhari ya habari hii. Kulikuwa na giza na utulivu. Ghafla pakawa na sauti za miguu ya askari wenye silaha wakitembea. Je, Petro na rafiki zake waliwaza nini wakati huo?<br>• Kwa ghafla, Yuda akijitokeza kwenye lile kikundi, akaja na kumbusu Yesu. *Elezea Yuda alikuwa nani na kuwa alimbusu Yesu ili kuwaonesha wale askari Yesu alikuwa ni yupi. Elezea “kusaliti” kunamaanisha nini (Angalia masomo ya daraja la pili)* ***(Mathayo 26:47-50)***<br>• Petro alipoona Yesu anakamatwa, akawa na hasira kubwa na akataka kumtetea Yesu kwa kumshambulia mtu mmoja katika kundi lile. ***(Mathayo 26:51)*** *Ni rahisi kwetu kupatwa na hasira kama Petro. Pendekeza mfano mmoja au miwili ambayo watoto wataielewa. Saa hiyo, Yesu akamwambia Petro aweke upanga wake mbali. Elezea kuwa, Yesu hakuhitaji kutetewa na Petro, kwa sababu alijua kuwa yote aliyokuwa anapitia yalikuwa ni mapenzi ya Mungu. Yesu alikuwa tayari kuwaruhusu adui zake kumkamata na kumuua. Alikuwa tayari kustahimili haya yote kwa ajili yetu. Elezea utofauti wa Petro na Yesu.* Yesu alikuwa na utulivu baada ya kumuomba Baba yake. Lakini Petro aliyeshindwa kuomba hakuweza kukabiliana na ile hali kama Yesu alivyotaka. ***(Mathayo 26:52-56)***<br>• Wale wanafunzi wakaogopa, wakamwacha Yesu na kukimbia. *Elezea kwa nini walifanya hivi.* ***(Mathayo 26:56b)*** Ni Petro tu aliyeamua kumfuata Yesu lakini kwa mbali na woga wa kukamatwa! *Wasaidie watoto kuwaza ni jinsi gani Petro angefanya hivi bila kugundulika.* ***(Mathayo 26:58)***<br>• *Elezea kuwa, kama sisi ni wafusi wa Bwana Yesu, tunaweza kumwomba ili atusaidie tusiwe watu wa hasira ila tuweze kujizuia. Roho Mtakatifu anayeishi kwenye maisha ya Mkristo ana uwezo wa kumsaidia kufanya mambo kwa njia inayofaa.*<br>• *Elezea jinsi gani tunaweza kushinda kama hatutafanya mambo kwa hasira na vita. Toa mifano.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Jesus prays in the Garden of Gethsemane. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Waefeso 4:26***. *Elezea kuwa, kama tumepatwa na hasira, ni vizuri kuiepuka kwa haraka!* |
| **KUMBUKA** | • Ni nani aliyekuja kwenye bustani akiandamana na maadui wa Yesu?<br>• Je, Yuda alifanya nini ili kuonesha Yesu alikuwa ni yupi?<br>• Je, Petro alitoa nini Yesu alipokuwa anakamatwa?<br>• Je, Petro alikata sehemu ipi ya mwili wa yule mtu?<br>• Je, Yesu alimwambia Petro afanye nini?<br>• Je, Mkristo atafanya nini ili kukabiliana na hasira?<br>• Je, wanafunzi walifanya nini Yesu alipokamatwa?<br>• Ni nani aliyejaribu kumfuata Yesu kwa mbali?<br><br>**Igiza:** Kiongozi wa darasa anaweza kuigiza sehemu moja au mbili ambapo mtu amepatwa na hasira kama ilivyoelezewa kwenye sehemu hiyo hapo juu. |

## <u>A4 Habari ya tatu</u>
## Petro akana – Habari hii inahusu uhitaji wa kusamehewa

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Wakati mwingine tunakosa ujasiri na kutowafurahisha marafiki<br>• Tunapomkosea Bwana Yesu, Yeye yu tayari kutusamehe kila wakati.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Zaburi 51:7***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mathayo 26:69-75*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Elezea jinsi gani tunawajua watu kwa sauti zao. Kama watoto wana uzoefu wa kutumia simu, wanaweza kujua ni nani anaongea kwenye simu bila ya kuambiwa. Elezea jinsi gani watu wanatamka maneno kwa utafauti na jambo hili linafanya sauti za watu kutofautiana. Unaweza kutoa mifano michache kutoka kwenye nchi ya Tanzania/Nchi yako.<br>• Jaribu kuunganisha habari hii na ile ya wiki iliyopita – wakumbushe watoto jinsi gani Yesu alikamatwa na wanafunzi wake walivyomkimbia. Petro naye alitaka kujua ni nini kitatokea. |
| **FUNDISHA** | • Petro alifuata hadi kwenye baraza la nyumba ya kuhani mkuu ***(Mathayo 26:69a)***. *Elezea sehemu ya nyumba inayoitwa baraza. Kama inawezekana, toa mfano wa nyumba yenye baraza.Tengeneza mandhari – usiku wenye baridi, moto, walinzi na wafanyakazi waliokuwepo hapo.*<br>• Kijakazi mmoja akamwona Petro na kumjua. Akawaambia wengine kuwa, Petro alikuwa pamoja na Yesu. Petro akasema kuwa, hajui yule kijakazi alikuwa anamaanisha nini. ***(Mathayo 26:69b-70)*** *Wasaidie watoto kuelewa kuwa, Petro alikuwa amesema uongo.* Ni kweli alikuwa pamoja na Yesu! *Jaribu kuangalia sababu zilizomsababisha Petro kusema uongo.*<br>• Baada ya Petro kuelekea kwenye malango, msichana mwingine akamjua. Kwa mara nyingine, Petro akasema hamjui Yesu. ***(Mathayo 26:71-72)*** *Kwa watoto wanaotumia masomo ya daraja la pili, elezea maana ya "kusaliti".*<br>• Baada ya muda mfupi, mtu mwingine akasema kuwa, Petro alikuwa anazungumza kama mmoja wa wanafunzi wa Yesu. (Petro, Yesu na wafuasi wengine walikuwa wametoka Galilaya. *Husisha maelezo haya na yale ya hapo awali kwenye utangulizi) Elezea jinsi gani Petro alikuwa amekasirika na kuogopa na kwa mara ya tatu akamkana Yesu.*<br>• Jogoo akawika na Petro akakumbuka maneno ya Yesu. ***(Mathayo 26:34)***. *Elezea kwa nini Petro alikasirika.* ***(Mathayo26:74b-75)***<br>• *Elezea kuwa, Petro alikuwa amefanya kosa. Hakuwa na ujasiri wa kusema kuwa, alikuwa mmoja wa wafuasi wa Yesu na badala yake akasema uongo. Sisi sote tunafanya makosa.*<br>• *Kuna wakati ambao pia sisi tunamkosea Bwana Yesu kwa matendo yetu. Bwana Yesu yu tayari kutusamehe. Ana uwezo wa kufanya hivyo kwa sababu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Peter denies Jesus. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Zaburi 51:7***. *Elezea kuwa, hili ni ombi. Unatuambia kuwa, tukimwomba Bwana Yesu atusamehe dhambi zetu, ni kama anatuosha na kutufanya safi kabisa – weupe kama dheluji. Elezea dheluji ni nini.* |
| **KUMBUKA** | • Petro alikuwa anasubiri wapi?<br>• Ni nani alikuwa mtu wa kwanza kuongea na Petro?<br>• Petro alimkana Yesu mara ngapi?<br>• Kwa nini Petro alisema uongo?<br>• Je, Petro alisikia jogoo akiwika mara ngapi<br>• Alikumbuka nini aliposikia jogoo akiwika?<br>• Kwa nini Petro alilia?<br>• Inatupasa kufanya nini tunapomkosea Bwana Yesu? |

## A4 Habari ya nne

**Petro apenda – Habari hii inahusu Petro na Yesu kufanya maongezi.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Petro alipewa fursa nyingine kuonesha upendo wake kwa Yesu baada ya kumkana.<br>• Bwana Yesu anataka tumpende.<br><br>**Mstari muhimu:** ***1 Yohana 4:19***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Yohana 21:1-19*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waambie watoto wajaribu kukumbuka habari za hapo awali kuhusu Petro. Kazi ya Petro ilikuwa ipi kabla ya Yesu kumwita?<br>• Elezea kuwa mengi yalikuwa yametokea wakati huo. Petro alikuwa mmoja wa marafiki wa Bwana Yesu lakini Petro alikuwa amemkosea Yesu (kumbuka habari tatu za hapo awali)<br>• Muda mchache baadaye, Yesu alikufa msalabani lakini akafufuka. Kwenye matukio mawili tofauti, Yesu alikutana na wanafunzi na kuwaonesha kuwa Yu hai! Siku moja baada ya haya kutokea, Petro akaamua kwenda kuvua samaki tena. |
| **FUNDISHA** | • Wanafunzi walikuwa wamevua usiku kucha bila ya kupata chochote! ***(Yohana 21:3)*** *Elezea jinsi gani walijihisi – kuchoka, wenye njaa na kukata tamaa.*<br>• *Waza kuhusu mandhari hiyo – jua la mapema asubuhi, mtu akiwa amesimama ufukweni. Fikiria kuhusu mazungumzo ya wanafunzi na Yule mtu wasiomjua.* ***(Yohana 21:4-6a)***<br>• Walipotii maelekezo ya Yule mtu, wakapata samaki wengi (153). Kwa ghafla, Yohana akagundua kuwa Yule mtu lazima atakuwa ni Yesu. Petro alifurahi sana na akaruka kwenye maji na kuenda alikokuwa Yesu. ***(Yohana 21:7-8)***<br>• Yesu akawaandalia kifungua kinywa. ***(Yohana 21:9-14)*** *Elezea jinsi gani inapendeza kupata kifungua kinywa ufukweni mwa bahari na jinsi gani ilikuwa maalum na pasipo kutarajia kuwa pamoja na Yesu.*<br>• Baada ya kifungua kinywa, Yesu akazungumza na Petro. Mara tatu akamuuliza kama alikuwa anampenda. ***(Yohana 21:15-19)*** *Elezea jinsi gani, hii ilikuwa muhimu kwa Petro. Bwana Yesu akaonesha kuwa alikuwa amemsamehe Petro na alikuwa na kazi maalum kwa ajili yake. Kwa watoto wa daraja la pili, unaweza kuelezea jinsi gani Petro alikuwa anaonesha upendo wake kwa Yesu mara tatu kinyume na alivyomkana hapo awali.*<br>• *Wape watoto changamoto kuhusu upendo wao kwa Yesu.*<br>• *Je, wangejibu vipi lile swali ambalo Bwana Yesu alimuuliza Petro? Yesu anataka kila mmoja wetu kumpenda na kumtumikia.*<br>• *Mungu alitupenda na akaonesha upendo wake kwa kumtuma Mwana Wake aje atuokoe. Inatupasa kumpenda pia.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Jesus appears to the Disciples in Galilee, Jesus questions Peter. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na elezea Mstari muhimu – ***1 Yohana 4:19*** |
| **KUMBUKA** | • Petro na rafiki zake walikuwa wemevua kwa muda upi?<br>• Waliambiwa washushe nyavu zao kilindini muda upi?<br>• Je, walivuwa samaki wangapi?<br>• Ni nani alikuwa wakwanza kugundua kuwa Yule mtu alikuwa Yesu?<br>• Ni nani alitaka awe wa kwanza kumuendea Yesu?<br>• Je, Petro alifanya nini kabla ya kuruka kwenye maji?<br>• Ni nani aliyeandaa kifungua kinywa?<br>• Je, walikula nini?<br>• Je, Yesu alimuuliza Petro swali lipi mara tatu?<br>• Je, Mstari muhimu unapatikana wapi?<br><br>**Igiza:** Baadhi ya sehemu za habari hii zinaweza kuigizwa (kwa mfano, kuvua samaki, kumwona mtu wasiomjua ufukweni, kuruka kwenye maji, kuvuta wale samaki kutoka baharini, kuhesabu wale samaki) na pia kuonesha kwenye uso (kwa mfano, kutoridhika, kushtuka, kufurahi...........). Inaweza kuwa mwafaka zaidi kusoma ile habari kutoka kwenye Biblia na kuwaomba watoto kuigiza kwenye sehemu husika. |

## A5 Habari ya kwanza

**Abramu aondoka nyumbani – Habari hii inahusu Abramu akimwamini Mungu.**

**Tunajifunza kuwa:**

- Abramu alimtii Mungu na akaondoka Uru na kuhamia nchi mpya.
- Inatupasa kuonesha tunamwamini Mungu kwa kumtii.

**Mstari muhimu:** ***Mithali 3:5***
**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 12:1-9***

### TOA UTANGULIZI

- Zungumza kuhusu kuhama kutoka kwenye nyumba moja kwenda nyingine, kama watoto wataweza kuelewa vizuri.
- Je, wangehisi vipi kwenda kuishi kwenye nchi nyingine mbali na nyumbani? – Wangefurahia? Wangekuwa na wasi wasi? Wangekuwa na huzuni? Toa sababu.
- Toa utangulizi wa Abramu. Elezea maisha yake yalikuwa ya namna gani huko Uru – Elezea kuhusu familia yake, rafiki zake, nyumba, wanyama, utajiri..... alikuwa na maisha mazuri!

### FUNDISHA

- Siku moja, Mungu akamwambia Abramu, "Toka wewe katika nchi yako na uende mpaka nchi nitakayokuonesha." ***(Mwanzo 12:1)*** *Je, nini kilikuwa kigumu kwa yale ambayo Mungu alikuwa anamwambia Abramu? (kuacha maisha yake mazuri/ bila kujua alikokuwa anaenda)*
- Mungu alimpa Abramu ahadi. ***(Mwanzo 12:2-3)*** *Elezea kuwa, ahadi za Mungu zilikuwa nzuri – Kwa mfano, taifa na jina kuu. Alitaka kumbariki Abramu. Mungu anapombariki mtu, anamuonesha wema wake.*
- Abramu alimtii Mungu. ***(Mwanzo 12:4)*** *Je, kwa nini Abramu alimtii Mungu? (Aliamini ahadi za Mungu/alimwamini Mungu)*
- *Elezea ni nani alikuwa na Abramu – Sarai mke wake na Lutu mwana wa nduguye, watumishi wake, na pia Mungu alikuwa pamoja naye ili kumuongoza. Elezea jinsi gani walisafiri kwa kutumia ngamia na kuishi hemani kwenye safari hii ndefu jangwani.*
- Mwishowe, Abramu akafika Kanani. ***(Mwanzo 12:6-9)***
- *Je, Abramu alihisi nini sasa? Elezea kuwa, Abramu alimshukuru Mungu kwa kujenga madhabahu.*
- *Elezea kuhusu hali ambazo Mungu anataka tumuamini tunapozipitia.*
- *Elezea kuwa, hii inamaanisha kumwamini Mungu kikamilifu, tunatarajia afanye mambo yawe sawa badala ya kutegemea njia zetu au uwezo wetu.*

**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**
**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Abraham moves to Canaan.

### JIFUNZE

Fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Mithali 3:5***. *Elezea kuwa, mstari huu unaelezea Abramu alifanya nini –alimwamini Mungu kwa moyo wake wote badala ya kufanya vitu kwa njia yake mwenyewe.*

### KUMBUKA

Tumia maswali yafuatayo yenye majibu ya, Ndiyo/Hapana ili kusisistiza habari hii na mafunzo yake. Wape chemsha bongo!

- Mungu alinena na Abramu.
- Abramu alitoka nyumbani kwa sababu ya njaa.
- Mungu aliahidi kumbariki Abramu.
- Abramu alikuwa na umri wa miaka 70 alipotoka nyumbani.
- Abramu alifahamu alikokuwa anaenda.
- Abramu alikuwa na mwana kwa jina Lutu.
- Mungu alimwongoza Abramu hadi Kanaani.
- Abramu aliishi kwenye nyumba katika nchi hiyo mpya.
- Abramu alimwamini na kumtii Mungu.
- Mungu anataka tumtii na tumwamini.

## A5 Habari ya pili

**Abramu na Lutu – Habari hii inahusu uchaguzi wa kichoyo wa Lutu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Lutu alifanya uchaguzi wa kichoyo uliotokea kuwa uchaguzi mbaya.<br>• Ni muhimu kwetu kufanya maamuzi sahihi.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Wafilipi 4:19***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 13:1-18*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Zungumza kuhusu maamuzi ambayo watoto wanafanya na pia kuhusu kuwaachia wengine fursa ya kuchagua kwanza. Chagua mfano mwafaka kwenye nchi au kabila lako.<br>• Zungumza kuhusu ugomvi na jinsi gani unaharibu mahusiano au urafiki. |
| **FUNDISHA** | • Watumishi wa Abramu na Lutu walikuwa na ugomvi kuhusu sehemu ya malisho kwa ajili ya mifugo yao. ***(Mwanzo 13:5-7)***<br>• Abramu alijua kuwa, ugomvi huo hautaleta mema kwa hivyo akampa Lutu nafasi ya kwanza kuchagua sehemu ya ardhi kwa ajili ya mifugo yake ***(Mwanzo 13:8-9)***<br>• *Elezea picha ya sehemu ile ukionesha tofauti iliyokuwepo mbele ya Lutu* – Lile bonde karibu na Yordani mahali palipokuwa na majani mengi mazuri ikilinganishwa na nchi ya milima ambayo haikuwa nzuri kwa muonekano wake. Je, unafikiri Lutu alichagua wapi?<br>• Uchaguzi wa Lutu. ***(Mwanzo 13:10-13)*** *Kwa nini Lutu alichagua sehemu aliyoichagua? (Aliona sehemu iliyopendeza na alitaka iwe yake). Lutu alikuwa ameingiwa na tamaa na ubinafsi kama sisi tunavyoweza kuwa. Elezea kuwa, sehemu aliyoichagua Lutu haikuwa nzuri kama alivyotazamia kwa sababu wale watu wa sehemu hiyo hawakumpendeza Mungu.*<br>• Abramu na Lutu wakatengana lakini Mungu alikuwa ameahidi kuwa, siku moja, angewapa Abramu na familia yake nchi yote ambayo anaiona kwa macho yake pande zote. ***(Mwanzo 13:14-18)***<br>• *Je, ungejihisi vipi kama ungekuwa Abramu? Je, ungehisi umedanganywa? (Sisitiza kuwa, Abramu alikuwa ana ahadi za Mungu ambazo ni zaidi ya uamuzi wa Lutu)*<br>• *Lutu alifanya uamuzi usiokuwa mzuri. Inatupasa kufanya uamuzi mzuri. Uamuzi mzuri zaidi tunaoweza kuufanya ni kumkaribisha Bwana Yesu katika maisha yetu na kusamehewa dhambi zetu.*<br>• *Sisitiza kuwa, Mungu anajua kilichochema kwenye maisha yetu na ana uwezo wa kutimiza mahitaji yetu kwa njia ya ukamilifu kama alivyompa Abramu kila alichokihitaji. Elezea kuwa, Mungu ni wakuaminika kwa sababu Yeye anaheshimu ahadi zake.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Abraham and Lot separate. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Wafilipi 4:19****, kwa kuihusisha na habari ambayo watoto wameisikia.* |
| **KUMBUKA** | Habari hii inakamilika wakati ambapo Abramu anajenga madhabahu. Mtu anayejibu maswali mengi na sahihi anapaswa kupata mawe mengi. ***(Mwanzo 13:1-6)*** Mawe halisi au ya kuchora yatafaa kwenye mchezo huu. Kikundi kitakachoshinda kitakuwa na mawe mengi zaidi ya kile kikundi/vikundi vingine.<br>• Je, tunajuaje kuwa Abramu alikuwa tajiri?<br>• Ni nani aliamua ugomvi uishe?<br>• Ni nani aliyechagua kwanza?<br>• Je, Lutu aliweza kuona mto upi?<br>• Je, Lutu alielekea upande upi?<br>• Ni kitu gani hakikuwa sawa sehemu ambayo Lutu aliichagua?<br>• Mungu alimwambia Abramu aangalie wapi?<br>• Je, Mungu alimuahidi Abramu nini? (Nchi na familia)<br>• Je, Abramu alifanya nini kwenye madhabahu aliyoijenga?<br>• Uamuzi muhimu zaidi katika maisha haya ni upi? |

## <u>A5 Habari ya tatu</u>

**Ahadi za Mungu kwa Abramu – Habari hii inahusu kuamini ahadi za Mungu.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Kwa sababu Mungu anajua maisha yetu ya baadaye, anaweza kuahidi hata mambo yatakayotokea.<br>• Mungu anataka tuamini ahadi zake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***1 Wakorintho 10:13 au Mwanzo 15:6***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 15:1-7*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Toa mfano wa ahadi unaoweza kutolewa kwa watoto. Elezea uaminifu wanaopaswa kuonesha wakati wa kungojea na ile furaha ya kutazamia ahadi kutimizwa. (Unaweza pia kutoa mfano wa ahadi ambayo haikutimizwa kwa sababu zisizoepukika)<br>• Kama wanadamu, wakati mwingine tunashindwa kutimiza ahadi zetu lakini Mungu kila wakati anatimiza ahadi zake! |
| **FUNDISHA** | • Mungu alinena na Abramu kwenye ndoto na akamuahidi mwana. ***(Mwanzo 15:1, 4)*** *Linganisha ahadi hii na ile ambayo tumejifunza hapo awali kuhusu Abramu. Jaribu kuonesha jinsi gani habari hii ilikuwa ya furaha kubwa kwa Abramu ambaye sasa alikuwa ana umri wa miaka zaidi ya tisini.*<br>• Mungu alimuonesha Abramu nyota na akamwambia kuwa, uzao wake utakuwa kama wingi wa nyota! ***(Mwanzo 15:5)*** *Fikiria jinsi ambavyo haiwezekani kuhesabu nyota! Wahusishe watoto kuhusu muujiza wa nyota na uumbaji wa Mungu.*<br>• Abramu aliamini ahadi ya Mungu. ***(Mwanzo 15:6)*** *Elezea kwa nini Abramu alimwamini Mungu.*<br>• Mungu alimpa Abramu na Sarai majina mapya. ***(Mwanzo 17:5, 15)*** *Jina jipya la Ibrahimu lina maana ya “baba wa mataifa mengi” kwa hiyo kila mara angekumbuka ahadi za Mungu.*<br>• *Mungu ana ahadi kwa ajili yetu kwenye Neno Lake, Biblia. Waambie watoto baadhi ya mifano ya ahadi za Mungu kwetu tunapomwamini.*<br>• *Mungu anafurahi tunapoamini anachokisema.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – God’s Promise to Abraham. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***1 Wakorintho 10:13*** (Mungu ni mwaminifu) – *Elezea kuwa, uaminifu unamaanisha kuwa, tunaweza kumtegemea Mungu kutimiza ahadi zake. Mwanzo 15:6 – Au elezea kuwa, Mungu alifurahi Abramu alipomwamini.* |
| **KUMBUKA** | • Mungu alikuwa amemuahidi Abramu atakuwa baba wa?<br>• Je, Mungu alimuahidi Abramu nini kwenye ndoto/maono?<br>• Mke wa Abramu alikuwa nani?<br>• Je, Mungu alimwonesha Abramu nini?<br>• Mungu alilinganisha nini na wingi wa nyota?<br>• Abramu alifanya nini Mungu alipompa ahadi hii?<br>• Jina jipya la Abramu lilikuwa?<br>• Jina jipya la Sarai lilikuwa?<br>• Mungu anataka tufanye nini tunapojifunza kuhusu ahadi zake kwetu?<br>• Neno “amini” linamaanisha nini? |

## A5 Habari ya nne

**Wageni wa Ibrahimu – Habari hii inahusu ahadi za Mungu kutimia.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu hutuma ujumbe wake kwa njia tofauti, hasa kabla Biblia haijaandikwa. Watu watatu muhimu walileta ujumbe wa Mungu kwa Ibrahimu.<br>• Mungu ni mwaminifu kwa ahadi zake –hakuna kitu kigumu kwake.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 18:14***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 18:1-15*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Elezea kinachotokea kwenye utamaduni wenu wakati ambapo wageni wanafika bila ya kutarajiwa. Unaweza kuigiza jinsi ya kukaribisha mgeni.<br>• Andaa mandhari ya kukaribisha wageni wa Ibrahimu – Ibrahimu alikuwa anapumzika mlangoni pa hema yake wakati wa mchana, alipowaona watu watatu mbele yake. Je, hawa walikuwa akina nani? |
| **FUNDISHA** | • Ibrahimu aliwakaribisha wageni wake na akaanda chakula na maji kwa ajili yao. ***(Mwanzo 18:2-8)*** *Elezea sehemu ya Sara. Onesha hisia unapoelezea habari hii – miale mizuri ya jua inayoangaza, maji ya baridi kwenye miguu iliyochoka, harufu nzuri ya chakula.*<br>• Baada ya kula, wale wageni wakampa Ibrahimu habari nzuri ya kuwa Sara atapata mtoto *wakati kama huo mwakani.* ***(Mwanzo 18:9, 10)*** *Je, wale wageni walijuaje haya? Elezea hawa wageni walikuwa ni akina nani – Watu wenye ujumbe wa Mungu kutoka mbinguni – mmoja alikuwa Bwana Yesu na wengine walikuwa malaika. Jadili kuhusu hisia za Ibrahimu kuhusu habari hii.* Ahadi za Mungu zilikuwa karibu kutimia!<br>• Sara alicheka kwa sababu alidhani ahadi hizo zilikuwa haziwezekani. Lakini Mungu aliahidi kufanya hayo ambayo kwa binadamu hayawezekani! ***(Mwanzo 18:11-15 )*** *Jadili jinsi gani Mungu alihisi Sara alipocheka.*<br>• Baada ya mwaka mmoja, mtoto wa Sara akazaliwa.***(Mwanzo 21:1-7)*** *Jaribu kufikiria kuhusu furaha waliyoipata. Je, Mungu alikuwa ametimiza ahadi yake? Kwa watoto wa daraja la pili, unaweza kuelezea maana ya jina Isaka. (Kicheko)*<br>• *Tunaweza kumtegemea Mungu atimize ahadi zote alizotupa. Hakuna kitu kigumu kwake – Yeye anatimiza ahadi hata siku za leo! Ni Mungu wa ajabu tunayemwamini!*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Abraham and the three strangers. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee Mstari muhimu – ***Mwanzo 18:14*** |
| **KUMBUKA** | Maswali haya yanahusiana na habari hii. Unaweza kuyatumia au kuwa na maswali mengine ya kwako mwenyewe kutoka kwenye habari zote nne za masomo ya A5.<br>• Wale Wageni walikuja saa ngapi siku hiyo?<br>• Ibrahimu alikuwa wapi wakati huo?<br>• Ibrahimu alimwomba Sara afanye nini?<br>• Je, walikuwa wale kitu gani kingine?<br>• Sara alikuwa wapi watu wale walipotoa habari hiyo?<br>• Kwa nini Sara alicheka?<br>• Sara angesubiria kwa muda gani mpaka kumpata mwanawe?<br>• Mtoto alipewa jina lipi?<br>• Ibrahimu alikuwa na umri gani Isaka alipozaliwa?<br>• Fikiria sababu mbili zilizowafanya Ibrahimu na Sara wawe na furaha. (Walipata mtoto, Mungu alikuwa ametimiza ahadi yake)<br><br>**Igiza:** Watoto watafurahia sehemu ya kwanza ya habari hii inapoigizwa. Igiza kwa ustadi. Watu wazima wanaosaidia watoto darasani wanaweza kuigiza sehemu ya Ibrahimu, Sara, watumishi, wale wageni watatu. Kwa njia nyingine, kwa kutumia kikundi kidogo, watoto wanaweza kuigiza kwa vitendo tu au kwa kusema maneno machache. |

## A6 Habari ya kwanza

**Ibrahimu amsikiliza Mungu – Habari hii inahusu kumpendea Mungu zaidi ya vyote.**

<table>
<tr><td></td><td>Tunajifunza kuwa:<br>• Ibrahimu alimpenda Mungu zaidi ya vyote au mtu yeyote.<br>• Inatupasa pia kumpenda Mungu kwa mioyo yetu yote.<br><br>Mstari muhimu: Mwanzo 22:8<br>Habari kwenye Biblia: Mwanzo 22:1-9</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>• Waulize watoto wakuambie baadhi ya mambo ambayo ni ya muhimu sana kwao – Ni kitu gani ambacho ni cha muhimu zaidi maishani mwako? Kwa nini ni cha muhimu?<br>• Kisha waulize wangehisi vipi kama ingewalazimu kuviachilia vitu hivyo – Je, ungependa kutoa kitu hicho? Je, ungejihisi vipi kama kingechukuliwa? Elezea kuwa, habari ya leo inahusu Ibrahimu kuachilia kitu kilichokuwa cha muhimu sana kwake.</td></tr>
<tr><td>FUNDISHA</td><td>• Mungu aliwatimizia Ibrahimu and Sara ahadi yake na akawapa mwana. Jina lake aliitwa Isaka na walimpenda sana. (Mwanzo 21:1-3)<br>• Siku moja, Mungu akamwambia Ibrahamu ampeleke Isaka kwenye mlima uitwao Moria. Inawezekana Isaka alikuwa kijana wa umri wa kati. Mungu alitaka Ibrahimu amtoa Isaka kama sadaka. Mungu alikuwa anamjaribu Ibrahimu ili kuona kama kweli alikuwa anampenda. Hata kama jambo hili lilimfanya Ibrahimu kuwa na huzuni kubwa, alimwamini Mungu na akafanya kama alivyoambiwa na Mungu. (Mwanzo 22:1-2) Ibrahimu alimpenda Mungu kwa moyo wake wote. Alimsikiliza Mungu na alikuwa tayari kumtii hata alipomwambia afanye kitu kilichokuwa siyo rahisi.<br>• Mapema asubuhi iliyofuata, Ibrahimu akaanda kila kitu kwa ajili ya safari. Akakata kuni kwa ajili ya sadaka na akaandamana na watumishi wawili na punda. (Mwanzo 22:3)<br>• Baada ya siku tatu, wakafika kwenye ule mlima ambao Mungu alikuwa ameuchagua. Ibrahimu akawaambia wale watumishi wawili wamsubirie na yule punda. Isaka akabeba kuni na baba yake akabeba kisu na moto. (Mwanzo 22:4-6)<br>• Walipoanza kukwea ule mlima, Isaka akamuuliza baba yake, “yuko wapi mwana-kondoo kwa ajili ya sadaka?” Ibrahimu akajibu, “Mungu atajipatia mwana-kondoo.” (Mwanzo 22:7-8)<br>• Ibrahimu alimtii Mungu kwa sababu alimpenda. Mungu anataka tumpende kwa mioyo yetu na kumtii kwa kila kitu anachotuambia tufanye.<br><br>Kamilisha somo la Wakati na Biblia.<br>Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa FBI – Abraham and Isaac.</td></tr>
<tr><td>JIFUNZE</td><td>Kama inafaa, fundisha na uelezee, Mstari muhimu – Mwanzo 22:8</td></tr>
<tr><td>KUMBUKA</td><td>• Mwana wa Ibrahimu aliitwa nani?<br>• Je, ni kwenye mlima upi ambao Mungu alitaka Ibrahimu aende?<br>• Je, Ibrahimu aliambatana na watumishi wangapi?<br>• Je, Ibrahimu aliенda kwenye ile safari na mnyama yupi?<br>• Je, walitumia siku ngapi kufikia ule mlima?<br>• Ni nani ambaye Ibrahimu alisema “Atajipatia mwana -kondoo”?<br>• Ni nani ambaye Ibrahimu alimpenda zaidi ya kila mtu na kila kitu?<br>• Ni nani ambaye inatupasa kumpenda kwa mioyo yetu yote?</td></tr>
</table>

**A6 Habari ya pili**

**Ibrahimu amtii Mungu – Habari hii inahusu kondoo dume achukua nafasi ya Isaka.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mungu alijipatia kondoo dume achukue nafasi ya Isaka.<br>• Yesu alichukua nafasi yetu alipokufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Wagalatia 2:20***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 22:9-14*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waambie watoto wafikirie kuwa, wanataka kuadhibiwa kwa kitu kibaya walichokifanya – Je, wangejihisi vipi?<br>• Kisha waambie watoto kuwaza kuwa, mtu mwingine alichukua ile adhabu kwa niaba yao– Je, wangehisi nini?<br>• Eleza watoto kuwa, habari ya leo inahisu kitu kingine kuchukua nafasi ya Isaka. |
| **FUNDISHA** | Wakumbushe watoto habari hii ilipoanza hadi sehemu tuliyopo sasa.<br>• Mwishowe, Ibrahimu na Isaka wakafika kwenye kilele cha mlima, mahali ambapo walijenga madhabahu ya mawe. Isaka akalazwa juu ya madhabahu hiyo. ***(Mwanzo 22:9-10)***<br>• Ibrahimu alipokuwa karibu kumtoa Isaka kama dhabihu kwa Mungu, malaika akanena na Ibrahimu kutoka mbinguni na akamwambia asimdhuru mwanawe. Ibrahimu alikuwa sasa ameonesha jinsi gani alikuwa anampenda Mungu. ***(Mwanzo 22:11-12)***<br>• Ibrahimu akatazama juu na akaona kondoo dume amenaswa pembe zake katika kichaka. Akamweka yule kondoo madhabahuni badala ya Isaka. ***(Mwanzo 22:13)***<br>• *Je, Ibrahimu na Isaka walijihisi vipi walipogundua kuwa, yule kondoo alikuwa achukuwe nafasi ya Isaka?*<br>• *Yesu alipokufa msalabani, alichukua nafasi yetu. Sote tumefanya mambo mabaya lakini Yesu alichukua adhabu ya maovu hayo alipotufia msalabani.*<br>• *Yesu alitufia kwa sababu anatupenda na hataki tuangamie kwa ajili ya dhambi zetu. Anataka nasi pia tumpende na kumshukuru kwa kuchukua nafasi yetu.*<br>• *Je, unahisi vipi kujua kuwa Yesu alikupenda kiasi cha kufa kwa ajili yako?*<br>• *Je, ni vipi tutamwonesha Yesu kuwa tunampenda*?<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Abraham and Isaac. |
| **JIFUNZE** | Kama inafaa, fundisha na uelezee ule Mstari muhimu – ***Wagalatia 2:20*** |
| **KUMBUKA** | • Ibrahimu alitengeneza madhabahu wapi?<br>• Je, walitumia nini kujenga ile madhabahu?<br>• Ni nani aliyemwita Ibrahimu kutoka mbinguni?<br>• Je, malaika alimwambia nini Ibrahimu?<br>• Je, Ibrahimu alimwonesha Mungu nini?<br>• Ni nini kilichukuwa nafasi ya Isaka madhabahuni?<br>• Ni nani alichukua nafasi yetu msalabani?<br>• Kwa nini Yesu alikufa msalabani? |

## A6 Habari ya tatu

**Msaada wa Mungu – Habari hii inahusu Mungu kuonesha njia.**

| | |
|---|---|
| | **Tunajifunza kuwa:**<br>• Mtumishi alimwomba Mungu msaada Naye akamsaidia.<br>• Mungu atatusaidia tukimwomba msaada.<br><br>**Mstari muhimu:** ***Mathayo 7:7***<br>**Habari kwenye Biblia:** ***Mwanzo 24:1-28*** |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waambie watoto wafikirie kuhusu watu wanaowasaidia – Wanaokusaidia? Je, wanakusaidia kufanya nini? Je, unajihisi vipi wanapokusaidia?<br>• Wape watoto fursa ya kusimulia jinsi gani walimsaidia mtu.<br>• Elezea watoto kuwa, habari ya leo inahusu Mungu kumsaidia mtu. |
| **FUNDISHA** | • Ibrahimu alikuwa mzee lakini kabla hajafa, alitaka kuwa na uhakika kuwa Isaka atafurahia ndoa yake. Kwa hiyo akampa mtumishi wake mkuu maagizo ya kumtafutia mwanawe mke. Alimwambia amwamini Mungu amuongoze kwa mwanamke sahihi. ***(Mwanzo 24:1-9)*** *Je, unafikiri yule mtumishi alihisi nini Ibrahimu alipomwambia amtafutie Isaka mke?*<br>• Yule mtumishi akawachukua ngamia kumi wa Ibrahimu na akaanza safari. Baada ya kusafiri kwa siku nyingi, akasimama karibu na kisima kwenye mji wa Nahori. Ulikuwa ni wakati wa jioni na mabinti walikuwa wanaenda kisimani kuteka maji. ***(Mwanzo 24:10-11)***<br>• Yule mtumishi akamwomba Mungu na kumuuliza amuoneshe kama kati ya hawa mabinti kuna mmoja atayekuwa mke wa Isaka. Angewaomba maji ya kunywa na binti ambaye angempa maji na pia kunywesha ngamia wake kumi ndiye atakayekuwa amechaguliwa na Mungu kwa ajili ya Isaka. ***(Mwanzo 24:12-14)***<br>• Baadaye akamwona binti mzuri sana akija kisimani. Jina lake aliitwa Rebeka. Alipomwomba maji ya kunywa, kwa furaha akampa na akawanywesha ngamia maji ya kutosha. *Je, yule mtumishi alikuwa anawaza nini? Je, alijihisi nini?* ***(Mwanzo 24:15-21)***<br>• Baada ya kumpa zawadi kutoka kwa bwana wake Ibrahimu, akamuuliza kama walikuwa na nafasi kwenye nyumba yao ambapo angekaa kwa muda. Aliposema kuwa wana nafasi ya kutosha, yule mtumishi akainama na kumshukuru Mungu kwa kuyajibu maombi yake na kumsaidia kumpata binti sahihi. ***(Mwanzo 24:22-27)***<br>• *Je, umewahi kupewa jukumu zito? Pendekeza mifano mwafaka.*<br>• *Je, yule mtumishi alimwomba nani msaada?*<br>• *Je, ni nani ambaye tunaweza kumwomba atusaidie? Mungu anataka kutusaidia na kutuongoza tunapokuwa na maamuzi ya kufanya. Atatusaidia kuchagua vilivyo sahihi.*<br><br>**Kamilisha somo la Wakati na Biblia.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa** FBI – Abraham and Isaac. |
| **JIFUNZE** | Fundisha na uelezee, ambapo panastahili, ule Mstari muhimu – ***Mathayo 7:7*** |
| **KUMBUKA** | • Ni nani aliyeenda kumtafuta mke kwa ajili ya Isaka?<br>• Je, yule mtumishi alienda safarini na ngamia wangapi?<br>• Je, yule mtumishi alisimama wapi?<br>• Ulikuwa wakati gani wa siku alipofika pale kisimani?<br>• Je, yule mtumishi alimwomba nani amsaidie kupata binti sahihi?<br>• Yule binti kisimani aliitwa nani?<br>• Je, alifanya nini ili kumsaidia yule mtumishi?<br>• Yule mtumishi alifanya nini alipojua kuwa Mungu amemsaidia?<br><br>Kama kuna muda, watoto wanaweza kuchora picha zao wakimsaidia mtu. |

**A6 Habari ya nne**

**Chaguo la Mungu – Habari hii inahusu Isaka kumwoa Rebeka.**

<table>
<tr><td></td><td>Tunajifunza kuwa:<br>• Rebeka na Isaka walifuata mpango wa Mungu na walikuwa na furaha sana.<br>• Tunapomwamini Mungu na kufuata njia zake, tutapata furaha.<br><br>Mstari muhimu: Zaburi 144:15<br>Habari kwenye Biblia: Mwanzo 24:28-67</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>• Uliza watoto kama wamewahi kwenda kwenye harusi – Ni nani aliyekuwa anaoa au kuolewa? Je, walivaa nini? Je, nini kilitendeka harusini? Je, Bibi na Bwana harusi walikuwa na furaha?<br>• Waambie watoto kuwa, habari ya leo inahusu harusi iliyofanyika nyakati za Biblia. Inawezekana habari hii inautofauti na jinsi harusi inavyoandaliwa hapa Tanzania.</td></tr>
<tr><td>FUNDISHA</td><td>Wakumbushe watoto habari hii ilipoanza hadi sehemu tuliyopo sasa.<br>• Rebeka akakimbia nyumbani na kuwaambia familia yake kilichotokea. Kaka yake Labani akakimbia kisimani na akamleta na kumkaribisha yule mtumishi nyumbani kwao. Lakini kabla yule mtumishi hajapata chakula cha jioni, akawaambia familia ya Rebeka sababu ya kuwajia. (Mwanzo 24:28-49)<br>• Baba yake pamoja na Labani wakakubaliana kuwa ni Mungu aliyekuwa amemwongoza huyo mtumishi kwa Rebeka. Bila kupoteza muda, wakamruhusu yule mtumishi kumchukua Rebeka awe mke wa Isaka. Yule mtumishi akamshukuru Mungu kwa kujibu maombi yake. Kisha akawapa Rebeka pamoja na familia yake zawadi nyingi. (Mwanzo 24:50-53)<br>• Asubuhi, wakamuuliza Rebeka kama angeenda na yule mtumishi na kuwa mke wa Isaka. Rebeka akakubali kwenda. (Mwanzo 24:54-61) Je, Rebeka alihisi vipi? (labda aliogopa kidogo kwa sababu hakumjua Isaka na familia yake lakini alifurahi kwa sababu huu ulikuwa ni mpango wa Mungu kwa ajili yake!)<br>• Kule nyumbani kwa Ibrahimu, Isaka alikuwa anasubiri na kutafakari kilichokuwa kinaendelea. Jioni moja alipokuwa anatembea, akaona ngamia wakija. Baadaye akamkaribisha Rebeka kwenye familia yake mpya na kampeleka kwenye hema ya mama yake. Isaka alimpenda Rebeka sana na akawa mke wake. (Mwanzo 24:61-67)<br>• Je, unafikiri Isaka alihisi vipi alipomwona mkewe kwa mara ya kwanza? (Inawezekana alikuwa na furaha kubwa na pia wasiwasi kidogo kwa sababu alikuwa hajawahi kukutana na Rebeka hapo awali. Lakini aliamini mpango wa Mungu pia na akafurahi kumchukua Rebeka kama mke wake).<br>• Isaka na Rebeka walifurahi sana kwa sababu walikuwa wamemwamini Mungu na kufuata mpango wake. Mungu anataka tumwamini pia na kufuata mpango wake. Tunapofanya hivi, tunajawa na furaha.<br><br>Kamilisha somo la Wakati na Biblia.<br>Onesha: Tafuta kwenye mtandao wa FBI – A wife for Isaac.</td></tr>
<tr><td>JIFUNZE</td><td>Fundisha na uelezee Mstari muhimu – Zaburi 144:15. Mstari huu unaelezea jinsi gani tutafurahi Mungu anapotimiza mipango yake kwenye maisha yetu.</td></tr>
<tr><td>KUMBUKA</td><td>• Je, kaka yake Rebeka aliitwa nani?<br>• Je, yule mtumishi alifanya nini kabla ya kula chakula cha jioni?<br>• Kwa nini familia ya Rebeka walikubali awe mke wa Isaka?<br>• Je, yule mtumishi aliwapa nini Rebeka na familia yake?<br>• Je, walisema ni nani aliyekuwa amemwongoza yule mtumishi kwa Rebeka?<br>• Je, ni wakati gani Rebeka aliondoka na yule mtumishi?<br>• Ni nani aliyekuwa anatembea kondeni wakati ambao Rebeka na mtumishi walifika nyumbani?<br>• Kwa nini Isaka na Rebeka waliishi kwa furaha?<br>• Ni nani ambaye atatufanya tuwe na furaha zaidi ya kila kitu au watu wote?</td></tr>
</table>

# Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**MASOMO YA DARAJA LA KWANZA:**

- Kurasa moja (au mbili kwenye kijitabu) kina sehemu za kupaka rangi au kujaza maneno machache kila wiki.
- Alama kumi zimewekwa kwa kila wiki na alama 40 kwa kila mwezi.
- Watoto wanaotumia masomo ya Daraja la kwanza hawatarajiwi kuwa wanajua kusoma vizuri. Hivyo basi, tunatarajia wazazi/ walezi/ viongozi wa madarasa kuwasaidia.
- Tumeweka alama 2 kwa kila jibu na hizo zilizobaki ili kuwa kumi ni kwa ajili ya maswali ya kupaka rangi. Jumla alama 10 kwa kila somo/ habari.

**MASOMO YA DARAJA LA PILI:**

- Kurasa mbili kila wiki.( au nne kwenye vijitabu)
- Habari ya Biblia ipo kwenye somo. Watoto/ wanafunzi wanapaswa kupata baadhi ya maneno kwenye somo, kupaka rangi, kukamilisha Mstari muhimu na kadhalika.
- Alama 20 zimewekwa kwa kila wiki na alama 80 kila mwezi masomo yanapokamilishwa kwa usahihi.

**KUSAHIHISHA MASOMO YA WAKATI NA BIBLIA**

**VITU VYA KUTUSAIDIA TUNAPOSAHIHISHA**

Waalimu wanaombwa kwanza:

- Kuangalia kila somo na kusahihisha ipasavyo.
- Toa alama kama ulivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia wino wa rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini hakuna alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama nusu kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uziandike kwenye nafasi uliyopewa kwa ajili hiyo.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.

Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**DARAJA LA KWANZA**

**Maoni ya jumla**

“Neema – Ninafurahi kuwa umeanza masomo haya na natumai unayafurahia. Nimependa sana ulivyopaka rangi.

“Je, huwa unaenda shule? Niambie kuhusu shule yako. Ninatarajia kusikia kutoka kwako siku za karibuni.”

“Hongera sana Pendo! Umepaka rangi kwa ustadi kweli! Je, ilikuwa vigumu kupaka rangi ndani ya picha tu? Ulikosea kidogo ulipokuwa unapaka rangi kwenye baadhi ya sehemu za somo la mwisho.”

**Maoni ya Kiroho**

“Umefanya vyema sana Faraja! Jairo alikuwa na furaha kubwa Yesu alipomsaidia.”

“Jibu zuri sana! Habari ya kifo cha Yesu inahuzunisha lakini cha kufurahisha ni kwamba, alifufuka tena.”

**DARAJA LA PILI**

**Maoni ya jumla**

“Jibu zuri sana Wema!– “Ninauhakika kuwa, walimu wako wanafurahia sana kazi zako huko shuleni!”

“Debora, naona kuwa tutasherehekea siku yako ya kuzaliwa hivi karibuni. Je, una maandalizi yoyote ya siku hiyo? Je, ni maadalizi gani? Uwe na siku njema!”

“Umejitahidi kweli. Lakini kuna makosa madogo. Usisahau kuhakiki majibu yako kila mara. Mtoto mzuri!”

**Maoni ya Kiroho**

“Napenda ulivyompaka rangi Mtoto Yesu akiwa horini. Je, si inapendeza sana Mungu kumtuma Yesu ulimwenguni kwa ajili yetu?”

“Napenda sana rangi ulizozitumia! Ilimbidi Zakaria kulipa gharama ya kutoamini maneno ya Mungu. Hakukosa kuamini maneno ya Mungu tena.”

“Majibu mwafaka kweli! Mtu aliyekutana na Filipo kule jangwani alienda akiwa na furaha kweli. Alisikia na kuamini Habari Njema za Yesu.”

© Bible Educational Services 2019

www.besweb.com

Registered Charity UK 1186004

Toleo la 01/2020